

WACHUNGAJI WATANGULIZI WAZAWA NCHINI TANZANIA

Re-arranged and translated by Pastor Stephen Letta

Lameck Marwa Chacha, (1943–2021)

Lameck Chacha Marwa alikuwa mchungaji na msimamizi nchini Tanzania.

Maisha ya Awali

Lameck Chacha Marwa alizaliwa Februari 2, 1943, katika Kijiji cha Kenyamanyori, wilayani Tarime, Mkoa wa Mara, nchini Tanzania. Baba yake alikuwa Marwa Nkaina, na mama yake alikuwa Mtatiro Chacha Marwa. Alikuwa mzaliwa wa kwanza kati ya ndugu zake; wengine walikuwa James Marwa Nkaina, Nyairabu Nkaina, na Wakuru Marwa Nkaina. Chacha aliamua kumpokea Yesu kama mwokozi wake binafsi na kujiunga na kanisa la Waadventista Wasabato kupitia ubatizo mwaka wa 1963.

Elimu na Ndoa

Chacha alisoma Shule ya Msingi Kibumaye wilayani Tarime mwaka 1955-1963, kisha akajiunga na Shule ya Sekondari Alliance iliyopo Musoma Mkoa wa Mara mwaka 1964 hadi 1968. Mwaka 1966 Marwa alimuoa Esther P. Marengo. Harusi ilifanyika katika kijiji cha Mtahuru wilaya ya Tarime Mkoani Mara. Lameck na mkewe walijaliwa watoto watano: Mwita William, Jane Gati, Nkaina Elia Chacha, Immanuel Werema, na Wegesa Ellen.

Mwaka 1971 Chacha alijiunga na Seminari ya Ikizu, iliyokuwa ikiendeshwa na Union Misheni ya Tanzania. Alihitimu mwaka 1972 na cheti cha uchunaji. Kuanzia 1980 hadi 1981 Lameck Chacha alihudhuria Chuo cha Ukumbusho cha Spicer nchini India, na kutoka 1982 hadi 1985 alihudhuria Chuo cha Waadventista cha Kusini (Southern Adventist College) nchini Marekani, na kuhitimu BA katika Theolojia. Alihudhuria Chuo Kikuu cha Jimbo la Jacksonville kutoka 1985 hadi 1987, na kuhitimu Shahada ya Uzamili katika Utawala wa Biashara.

Uchungaji

Mchungaji Lameck Chacha alipitia magumu ili kuwa Muadventista, wa kwanza katika familia yake kufanya hivyo. Wanafamilia wote, akiwemo baba yake, walikataa yeye kujiunga na kanisa. Safari yake katika huduma ilianza kama mwinjilisti wa vitabu wa muda (part time), alipokuwa akifanya kazi katika Hospitali ya wilaya ya Tarime kama nesi kuanzia mwaka 1966 hadi 1969. Mwaka 1973 Konferensi ilimwita kuhudumu katika mtaa wa Kinesi kama mchungaji wa Mtaa. Kuanzia 1973 hadi 1977 Chacha alihudumu katika mtaa wa Kibumaye kama mchungaji wa mtaa. Mnamo 1978 alihudumu katika mtaa wa Salagana kwa miezi minane. Alipata kuwa Meneja wa Kituo cha Vitabu cha Waadventista cha Mara Field mwaka 1980. Kuanzia 1989 hadi 1990 alihudumu katika Union Misheni ya Tanzania kama mhasibu. Mwaka 1991, Mkutano wa Mara ulimchagua kuwa Mwenyekiti wa Konferensi ya Mara kwa kipindi cha mwaka mmoja. Kuanzia 2005 hadi 2010 Mchungaji Chacha alihudumu kama mkurugenzi wa idara ya mawasiliano ya konferensi, mkurugenzi wa vijana na Chaplain wa konferensi.

WACHUNGAJI WATANGULIZI WAZAWA NCHINI TANZANIA

Re-arranged and translated by Pastor Stephen Letta

Maisha ya Baadaye

Mchungaji Chacha alistaafu utumishi mwaka 2010 katika Konferensi ya Mara alipokuwa mkurugenzi wa mawasiliano. Ingawa Mchungaji Chacha alistaafu, aliendelea kushiriki katika shughuli za kanisa, hasa katika Kanisa la Waadventista wa Sabato Bima. Akiwa na mke wake, alichangia kununua kiwanja ambacho kanisa la Bima lilijengwa na kusaidia ujenzi wa kisima cha ubatizo cha kanisa hilo. Mwaka 2008 afya ya Mchungaji Chacha ilidhoofika kutokana na ugonjwa wa kisukari, na mwaka 2015 alipoteza uwezo wa kuona. Mwaka 2016 hadi 2019 alipata matatizo ya moyo na kulazwa katika Hospitali ya Mkoa wa Mara mara kadhaa kwa matibabu. Alifariki Machi 8, 2021 katika Hospitali ya Mkoa wa Mara, Tanzania. akiwa na umri wa miaka 78. Alizikwa katika kijiji cha Kebanga, wilayani Tarime, mkoani Mara, nchini Tanzania, Machi 15, 2021.

Mchango wake

Lameck Chacha Marwa anakumbukwa kwa kuanzisha uhamishaji wa Makao Makuu ya Konferensi ya Mara kutoka Busegwe hadi Musoma mjini, ambako usafiri wa pande zote unapatikana.